



## Baada ya uchunguzi wako wa mammogram, kitu gani kinafuata?

### Hongera kwa kufanyiwa uchunguzi huu muhimu wa afya!

Picha zako zitaweza kusomwa na watu wawili wapiga picha. Kila juhudi zimefanywa ili kuhakikisha kwamba matokeo yako yanatumwa kwa barua au kutumwa kielektroniki katika wiki mbili. Nakala pia itatumwa kwa GP ambaye utamchagua isipokuwa kama ukiomba vinginevyo. Kwa idhini yako matokeo ya uchunguzi wa Mammogram yatajumuishwa katika rekodi yangu ya afya. Kama una wasiwasi wowote unaweza kutembelea tovuti [www.breastscreen.health.wa.gov.au](http://www.breastscreen.health.wa.gov.au) au piga simu (08) 9323 6700 au simu za bure vijijini 1800 800 033.

### Inakuwaje kama ninahitaji kurudia X-ray?

Mara chache sana mpiga picha ataomba kurudia X-ray ikiwa picha hiyo haiko wazi vizuri. Kama hii ni muhimu, utapigiwa simu au kuandikiwa barua ikikuomba kurudi. Huku kurudia X-rays kutafanyika katika kliniki ya uchunguzi.

### Inakuwaje kama ninahitaji X-rays zaidi?

Wastani wa mwanamke 1 kati ya 20 huulizwa kurudi kwenye X-rays ya matiti zaidi. Hizi X-rays kuzingatia eneo la matiti ambalo linahitaji kuchunguzwa kwa undani zaidi. Ikiwa hii ni muhimu, BreastScreen WA itawasiliana na wewe kufanya miadi.

### Wanawake wanaoishi katika eneo la mji mkuu

Katika eneo la mji mkuu, X-rays zaidi hufanywa katika moja ya vituo vya tathmini ya matiti vya BreastScreen WA, vilivyoko katika hospitali ya Fiona Stanley, Royal Perth na Sir Charles Gairdner. Mara nyingi hizi X-rays za ziada huonyesha kuwa hakuna tatizo. Idadi ndogo ya wanawake wanahitaji baadhi ya vipimo vya zaidi, kama vile ultrasound au biopsy. Vipimo hivi vinafanywa katika siku hiyo hiyo kama X-rays ya ziada.

### Wanawake wanaokaa vijijini WA

Kwa wanawake wanaoishi vijijini, X-rays zaidi hufanyika katika huduma ya kuzunguka. BreastScreen WA itawasiliana na wewe kujua kama vipimo vyovyote vya ziada vitahitajika.

Kuna huduma ya kudumu ya uchunguzi ya kikanda na ya kutathmini katika Kituo cha Afya cha Bunbury Kusini Magharibi.

### Ni muhimu kukumbuka kwamba wanawake wengi ambao hufanya vipimo zaidi hawana saratani

Wanawake wote ambao wanahitaji vipimo zaidi na uchaguzi wa kuweza kurejeshwa moja kwa moja kwa vituo vya tathmini ya matiti au kuona GP wao. Matokeo yote ya vipimo katika vituo vya tathmini ya matiti hupatikana wakati wa miadi, isipokuwa matokeo ya msingi ya muhimu ambayo yatapatikana baada ya masaa 24.

Kwa wanawake wachache wenye saratani, ugunduzi wa mapema kwa kiasi kikubwa huboresha nafasi ya matibabu yenye mafanikio. Saratani ya matiti ndogo mara nyingi inaweza kutibiwa na upasuaji chini ya kina kuliko ile inayohitajika kwa saratani kubwa.

### Je mammogram itaonyesha saratani za matiti zote?

Uchunguzi wa mammograms unaweza kuchunguza 70-90% ya saratani ya matiti. Kuna, hata hivyo, idadi ndogo ya saratani ambayo haiwezi kuonekana kwenye uchunguzi wa Mammogram. Kuna uwezekano kwamba mammography inaweza kukosa mabadiliko kutokana na saratani ya matiti (uongo wa hasi) au kwamba vipimo zaidi vitafanyika ili kuchunguza mabadiliko ambayo hayatokani na saratani ya matiti (chanya ya uongo).

Kama wewe ukiona mabadiliko yoyote katika matiti yako kama vile vibonge, mchozo chuchu au maumivu mpya ya matiti, Tafadhali onana na GP wako mara moja, hata kama uchunguzi wa Mammogram wa mara ya mwisho ulionyesha kuwa hakuna dalili ya saratani ya matiti. Mabadiliko ya uvimbe, kama vile kiuvimbe, mara nyingi kuonekana kwenye uchunguzi wa Mammogram lakini itatolewa taarifa kwako kama tu vipimo zaidi vinahitajika.

## Kitu gani kinafuata baadaye?

BreastScreen WA itatuma barua kuonyesha ni lini unatakiwa kurudi kwenye uchunguzi wako wa Mammogram. Kama kwa sababu yoyote hutapokea barua, tafadhali tupigie simu 13 20 50\* na tutapanga miadi kwa ajili yenu.

Mammograms ambayo umewahi kuchukuliwa na programu hiyo huhifadhiwa kwa uangalifu kwa kulinganisha na skrini za matiti zijazo.

Wanawake wenye umri wa miaka 75 na zaidi hawapokei barua ya kukumbusha lakini wanakaribishwa kuomba miadi kwenye mtandaoni au simu 13 20 50\* kwa miadi.

Kama ukibadilisha anwani, tafadhali piga 13 20 50\* na kuweza kutujulisha.

Kwa huduma ya ukalimani 13 14 50

(\*kwa gharama za kawaida)

## Naweza kufanya nini?

**Wanawake wenye miaka Zaidi ya 50, wanapata vipimo vya BURE vya mammogram kila baada ya miaka miwili.**

- Ikiwa unapimwa mara kwa mara saratani ya matiti ambayo inaweza kugunduliwa badi inaweza kuwa katika hatua ya mwanzo.
- Ni kati ya asilimia 1 – 5 ya wanawake wanaweza kuhitaji uchunguzi wa kila mwaka wa kipimo cha Mammogram kulingana na umuhimu wa historia ya familia ya saratani ya matiti.
- Ikiwa umewahi kuwa na saratani ya matiti ni muhimu kuona GP wako kwa ajili ya kufuatilia na kuwa na uchunguzi wa kila mwaka wa kipimo cha Mammogram.

### Fahamu matiti

- Kupata kujua matiti yako na ni kitu gani cha kawaida kwako. Angalia katika kioo katika matiti yako na kufinya matiti yako mara kwa mara.
- Onana na GP wako mara moja ikiwa unaona mabadiliko yoyote yasiyo ya kawaida katika matiti yako.
- Muulize GP wako kuhusu afya ya matiti katika miadi yako ijayo.

### Mabadiliko ambayo lazima hayawezi kupuuzwa ni:

1. uvimbe, kuvimba au kubanwa katika matiti au ubavu;
2. mabadiliko katika chuchu kama vile miingilio, chuchu kutoa usaha, kuuma au ngozi kuwa na vidonda;
3. mabadiliko katika ngozi ya matiti kama vile chunusi, upele au uwekundu;
4. eneo la matiti ambayo linaweza kuonekana tofauti na pengine;
5. maumivu mapya ya matiti ya kuendelea.

## Je una swali lolote?

Wasiliana na GP wako au piga simu: BreastScreen WA on 13 20 50 kwa miadi au (08) 9323 6700 kwa habari au 1800 800 033 kupiga kwa bure kwa wanawake wa vijijini

Barua pepe: [breastscreenwa@health.wa.gov.au](mailto:breastscreenwa@health.wa.gov.au)

Huduma ya Taifa ya Kupunguza [www.relayservice.gov.au](http://www.relayservice.gov.au)

Huduma ya Ukalimani na Utafisiri (TIS) 13 14 50

**Habari Zaidi katika lugha yako zinapatikana katika tovuti ya BreastScreen WA website:**

[www.breastscreen.health.wa.gov.au/Breast-screening/Multicultural-women](http://www.breastscreen.health.wa.gov.au/Breast-screening/Multicultural-women)



[www.breastscreen.health.wa.gov.au](http://www.breastscreen.health.wa.gov.au)